OFISI YA MWANASHERIA
MKUU WA SERIKALI

# WIKI HII MAGAZETINI NA MITANDAONI

06/07/2025 ► 12/07/2025

OAG

HABARI KITAIFA

# Jaji Mkuu akabidhiwa Juzuu za Sheria

Na Mwandishi Wetu

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amemkabidhi Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu Toleo la mwaka 2023, Jaji Mkuu wa Tanzania, George Masaju, jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa kukabidhi juzuu hizo mwishoni mwa wiki, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alimshukuru Jaji Mkuu kwa mchango wa mahakama katika kufanikisha Urekebu wa Sheria.

Alisema kuanza kutumika kwa sheria hizo kutairahisishia mahakama wakati wa kutekeleza majukumu yake ya utendaji haki kwa wananchi. "Jaji Mkuu baada ya kukamilika urekebu na Rais Samia Suluhu Hassan alizindua na alitoa tamko kwamba sheria hizi zianze kutumika kuanzia Julai mosi, mwaka huu, hivyo tumekuja na timu yangu kukukabidhi rasmi juzuu hizi zilizofanyiwa urekebu," alisema Johari.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema, mradi wa urekebu wa sheria umefanyika kwa kutumia rasilimali za fedha za ndani na rasilimali watu wa ndani, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma wakati mradi huo ulipokuwa ukiendeshwa na wahisani.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema, mradi wa urekebu wa sheria umefanyika kwa kutumia rasilimali za fedha za ndani na rasilimali watu wa ndani, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma wakati mradi huo ulipokuwa ukiendeshwa na wahisani.

"Kitu kizuri ni kwamba huu mradi tumeufanya kwa fedha zetu za ndani na hata publisher (mchapishaji) ni wa ndani, kuanzia sasa hatutasubiri tena miaka kumi zile 'annual supplement' sasa tutahakikisha tunazitoa ipasavyo ili ikifika miaka 10 mradi usiwe mkubwa sana," alisema.

Akipokea juzuu hizo, Jaji Mkuu wa Tanzania, Masaju aliishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutambua mchango wa mahakama wa kufanikisha kazi hiyo na ameeleza kuwa mahakama ni mtumiaji mkubwa wa sheria hizo na zitasaidia katika utendaji kazi wa mahakama.

"Sisi kama mahakama ni moja ya watumiaji wakuu kwasababu mambo mengi yanaishia mahakamani hivyo tukiwa na hizi juzuu zitatusaidia sana," alisema.

Katika hatua nyingine, Jaji Mkuu wa Tanzania alipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuukamilisha mradi wa urekebu wa sheria kwa kutumia rasilimali fedha za ndani pamoja na kuzifanya sheria hizo kupatikana bure kwa njia ya mtandao na kuwasaidia watumiaji wengi kuzipata kwa urahisi.

Awali, Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole, alimpongeza Jaji Mkuu wa Tanzania kwa mchango wa kukamilisha urekebu tangu akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwamba wamekabidhi seti ya juzuu za sheria za nchi 20 zenye jumla ya sheria kuu 446.

Vilevile, Mwandishi Mkuu wa Sheria alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetekeleza maagizo ya Rais Samia ya kuhakikisha sheria hizo zinapatikana, katika mfumo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujulikanao kama OAG-MIS.

ria kuu 446.

Vilevile, Mwandishi Mkuu wa Sheria alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetekeleza maagizo ya Rais Samia ya kuhakikisha sheria hizo zinapatikana, katika mfumo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujulikanao kama OAG-MIS.

"Kama alivyoelekeza Rais Samia wakati wa uzinduzi kuwa sheria hizi ziwe 'accessible' pamoja kwa kupatikana kwa njia ya kuuzwa na mchapishaji Mkuki na Nyota na pia sheria hizi zinapatikana katika mfumo wa OAG-MIS wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali," alisema Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Juzuu za Sheria zilizofanyiwa urekebu toleo la mwaka 2023 zilitiwa saini na kutolewa tamko na Rais Samia Aprili 23, mwaka huu na zimeanza kutumika Julai mosi, mwaka huu.





oagtanzania
www.oag.go.tz

# Jaji Mkuu akabidhiwa Juzuu za Sheria

**Na Heri Shaaban**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, amemkabidhi Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la Mwaka 2023 Jaji Mkuu wa Tanzania George Masaju.

Akizungumza wakati wa kukabidhi Juzuu hizo wiki iliyopita, Johari,ameeleza kuwa kuanza kutumika kwa sheria hizo kutairahisishia Mahakama wakati wa kutekeleza majukumu yake ya utendaji haki kwa wananchi.

" Jaji Mkuu baada ya kukamilika kwa zoezi la urekebu na Rais alizindua na alitoa tamko kwamba sheria hizi zianze kutumika kuanzia Julai 1,2025, hivyo tumekuja na timu yangu kukukabidhi rasmi Juzuu hizi zilizofanyiwa Urekebu,"alisema Johari.

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza kuwa mradi wa urekebu wa sheria umefanyika kwa kutumia fedha za ndani na rasilimali watu wa ndani, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo mradi huo ulikuwa ukiendeshwa na wahisani.

Akipokea juzuu hizo, Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Masaju,ameeleza kuwa Mahakama ni mtumiaji mkubwa wa sheria hizo na zitasaidia katika utendaji kazi wake.

"Sisi kama Mahakama ni moja ya watumiaji wakuu kwa sababu mambo mengi yanaishia mahakamani hivyo tukiwa na hizi juzuu zitatusaidia,"alisema Masaju.

Katika hatua nyingine Jaji Mkuu wa Tanzania ameipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuukamilisha mradi wa urekebu wa sheria kwa kutumia rasimali fedha za ndani pamoja na kuzifanya sheria hizo kupatikana bure kwa njia ya mtandao na kuwasaidia watumiaji wengi kuzipata kwa urahisi.

Awali, Mwandishi Mkuu wa Sheria, Onorius Njole, alimpongeza Jaji Mkuu wa Tanzania kwa mchango wake katika kukamilisha zoezi hilo tangu akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambapo alisema wamekabidhi seti ya Juzuu za sheria za nchi 20 ambayo ina jumla ya sheria kuu 446.

Vilevile alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan,ya kuhakikisha Sheria hizi zinapatikana, ambapo sheria hizo zinapatikana katika mfumo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujulikanao kama OAG-MIS.

"Kama alivyoelekeza,Rais wakati wa uzinduzi kuwa sheria hizi ziwe zinapatikana kwa urahisi na kwa njia ya kuuzwa na mchapishaji Mkuki na Nyoto pia zinapatikana katika mfumo wa OAG-MIS wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,".

Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la mwaka 2023 zilisainiwa na kutolewa tamko na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan Aprili 23 , 2025 na zimeanza kutumika kuanzia tarehe Julai 1,2025.



**Jaji Mkuu wa Tanzania George Masaju akipokea juzuu zilizofanyiwa urekebu toleo la mwaka 2023 kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari(kulia) mwishoni mwa wiki. Juzu hizi za nchi 20 zina jumla ya sheria kuu 446** (Picha na Heri Shaaban)

# AG.Johari amkabidhi Jaji Mkuu Juzuu za sheria

**NA MWANDISHI WETU**

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali, Hamza S. Johari (pichani kulia) amemkabidhi Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la Mwaka 2023 Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji George M. Masaju (pichani kushoto) Ofisini kwake Jijini Dodoma Julai 3, 2025.

Akizungumza wakati wa kukabidhi Juzuu hizo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amemshukuru Jaji Mkuu kwa mchango ambao Mahakama imeutoa katika kufanikisha kazi ya Urekebu wa Sheria ambapo ameeleza kuanza kutumika kwa sheria kutarahisisha Mahakama wakati wa kutekeleza majukumu yake ya utendaji haki kwa wananchi.

"Mhe. Jaji Mkuu baada ya kukamilika kwa kazi ya urekebu na Mhe. Rais alizindua na alitoa tamko kwamba Sheria hizi zianze kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, hivyo tumekuja na timu yangu kuja kukukabidhi rasmi Juzuu hizi zilizofanyiwa Urekebu." Amesema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali amefafanua kuwa mradi wa urekebu wa sheria umefanyika kwa kutumia rasilimali za fedha za ndani na rasilimali watu wa ndani, tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo mradi huo ulikuwa ukiendeshwa na Wahisani.

"Kitu kizuri ni kwamba huu mradi tumeufanya kwa fedha zetu za ndani na hata publisher ni wa ndani, kuanzia sasa hatutasubiri tena miaka kumi ile annual supplement sasa tutakuwa tunatoa ipasavyo ili tufika miaka 10 mradi uwe mkubwa zaidi". Ameeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali.



Akipokea Juzuu hizo, Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji George M. Masaju ameishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutambua mchango wa Mahakama katika kufanikisha kazi hiyo, ambapo ameeleza kuwa Mahakama ni mtumiaji mkubwa wa sheria hizo na zitasaidia katika utendaji kazi wa Mahakama.

"Sisi kama Mahakama ni moja ya watumiaji wakuu kwenye hili mambo mengi yanatokea mahakamani hivyo tukitwa na hizi Juzuu zitatusaidia sana." Amesema Jaji Mkuu wa Tanzania.

Katika hatua nyingine Jaji Mkuu wa Tanzania amepongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kukamilisha mradi wa urekebu wa sheria kwa kutumia rasilimali fedha za ndani pamoja na kuifanya sheria hizo kupatikana bure kwa njia ya mtandao na kuwasaidia watumiaji wengi kuzipata kwa urahisi.

Awali, Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bw. Onorius Njole amempongeza Jaji Mkuu wa Tanzania kwa mchango wake katika kukamilisha zoezi hilo tangu akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambapo amesema wamekabidhi seti ya Juzuu za sheria za nchi 20 ambapo ina jumla ya sheria kuu 446.

Vilevile Mwandishi Mkuu wa Sheria amesema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Sheria hizi zinapatikana, ambapo sheria hizo zinapatikana katika mfumo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ujulikanao kama OAG-MIS.

"Kama alivyoelekeza Mh. Rais wakati wa uzinduzi kuwa sheria hizi ziwe accessible pamoja kwa kupatikana kwa njia ya kununua na mchapishaji Mkuki na Nyota na pia sheria hizi zinapatikana katika mfumo wa OAG-MIS wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali". Amesema Mwandishi Mkuu wa Sheria.

Juzuu za Sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la mwaka 2023 zilizinduliwa na kutolewa tamko na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 23 April, 2025 na zimeanza kutumika kuanzia Julai mosi, 2025.

# Ofisi ya AG kuendelea kuboresha ushauri taasisi za umma nchini

Na Heri Shaaban

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itaendelea kuboresha ushauri kwa taasisi za umma wakati wa kuingia mikataba mbalimbali ili kuwa na mikataba iliyoborana na inayotekelezwa vizuri na kuwanufaisha wananchi.

Hayo yamesemwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali,Samwel Maneno, katika Maonesho ya Kimataifa ya 49 ya Biashara ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Wilaya ya Temeke Mkoa wa Dar es Salaam.

"Tunaendelea kuzipa ushauri taasisi za umma ili kuwa na ubora wa mikataba pia kuhakikisha utekelezaji wa

mikataba hiyo unafanyika kwa mujibu wa Makubaliano," alisema Maneno.

Maneno alisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inayatumia maonesho hayo kutoa ushauri wa kisheria, kushughulikia malalamiko, utatuzi wa migogoro na elimu ya sheria hususani sheria zilizofanyiwa urekebu toleo la Mwaka 2023 zilizoanza kutumika Julai Mosi mwaka huu.

"Sheria zilizofanyiwa urekebu zimezinduliwa na zimeanza kutumika na kitu kizuri ni kuwa kati ya sheria 446 sheria 300 zinapatikana kwa lugha ya kiswahili"alisema.

Pia Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alipata fursa kutembelea mabanda ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na Taasisi ya Mafunzo ya uanasheria kwa vitendo, kuona shughuli zinazotekelezwa na taasisi hizo katika maonesho hayo.

Maonesho ya Sabasaba 2025 yamezinduliwa rasmi Julai 2025 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ambapo maonesho yanatarajiwa kumalizika Julai. 13, 2025.




**Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, . Samwel Maneno (kushoto) akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Huduma za Ushauri wa Kisheria Neema Ringo, katika Banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam. (Picha na Heri Shabani)**

# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali kuendelea kuboresha ushauri mikataba kwa Taasisi za umma

**NA MWANDISHI WETU**



OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuboresha Ushauri kwa Taasisi za Umma wakati wa kuingia mikataba mbalimbali ili kuwa na Mikataba iliyobora na kutimiza malengo ya Serikali ya kuwa na mikataba inayotekelezwa vizuri na kuwanufaisha Wananchi.

Hayo yamesemwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel M. Maneno Julai 7, 2025 katika Maonesho ya Kimataifa ya 49 ya Biashara ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

"Tunaendelea kuzipa ushauri Taasisi za Umma ili kuwa na ubora wa mikataba pia kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Mikataba hiyo unafanyika kwa mujibu wa Makubaliano". Amesema Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Aidha, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inayatumia maonesho hayo katika kutoa Ushauri wa Kisheria, Kushughulikia Malalamiko, Utatuzi wa Migogoro na Elimu ya Sheria hususani sheria zilizofanyiwa Urekebu toleo la Mwaka 2023 zilizoanza kutumika Julai 1, 2025.

"Sheria zilizofanyiwa urekebu zimezinduliwa na zimeanza kutumika na kitu kizuri ni kuwa kati ya sheria 446 sheria 300 zinapatikana kwa lugha ya kiswahili". Ameeleza Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Katika hatua nyingine Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitembelea mabanda ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, kuona shughuli zinazotekelezwa na Taasisi hizo katika maonesho hayo.

Maonesho ya Sabasaba 2025 yamezinduliwa rasmi leo tarehe 7 Julai, 2025 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ambapo maonesho yanatarajiwa kumalizika Julai 13, 2025.



oagtanzania
www.oag.go.tz

# WATANZANIA

## 10/07/2025

UCHAMBUZI / PICHA




*Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bw. Onorius Njole hivi karibuni alitembelea banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya Biashara ya 49 ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.*

oagtanzania




**oagtanzania** HABARI PICHA

Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro tarehe 11 Julai, 2025 ametembelea Banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

Aidha, Waziri wa Katiba na Sheria ameipongezea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushiriki kwenye Maonesho na kuendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya Kisheria kwa wananchi.

# Tanzania's Attorney General underscores legal education drive at Sabasaba Trade Fair

by THE RESPONDENT ONLINE - July 10, 2025 0

Advertisement

Tanzania's Attorney General,Hamza S. Johari, has reaffirmed the government's commitment to raising legal awareness among citizens, stating that public education is the central objective behind his office's participation in the 49th Dar es Salaam International Trade Fair (DITF), commonly known as Sabasaba.

Speaking during his visit to the Mwalimu Nyerere Fairgrounds, where the annual exhibition is taking place, Johari emphasized that the Office of the Attorney General is not only a legal advisor to the government but also a public-facing institution dedicated to providing accessible legal guidance.



Mtaa Kwa Mtaa
mtaakwamtaa.co.tz






# "LENGO KUU LA KUSHIRIKI MAONESHO HAYA NI KUTOA ELIMU KWA UMMA" – MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari amefanya ziara ya kutembelea maonesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Sabasaba Jijini Dar es Salaam, tarehe 10 Julai, 2025

Akizungumzia ushiriki wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika maonesho hayo Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema kuwa pamoja na masuala mengine Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashiriki maonesho hayo kwa lengo kuu la kutoa elimu ya masuala ya Kisheria kwa Wananchi.

"Lengo letu la kuja kwenye maonesho haya ni kutimiza moja ya malengo yetu, ambayo ni kutoa elimu kwa umma ili waweze kufahamu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama mshauri mkuu wa Serikali na kazi ambazo Ofisi hii inafanya". Amesema Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema kuwa sambamba na kutoa elimu kwa masuala ya kisheria kwa wananchi pia Ofisi hiyo inatoa huduma za utatuzi wa migogoro mbalimbali ya kisheria pamoja kushughulikia malalamiko mbalimbali ya wananchi.

MediaBrains
DEEP THINKERS

KITAIFA

# Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Kusimamia Ubora wa Mikataba ya Umma kwa Maslahi ya Taifa




Na Tatu Mohamed

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesisitiza dhamira yake ya kuendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi za umma ili kuhakikisha mikataba inayosainiwa na serikali inakuwa na ubora, inatekelezwa ipasavyo na inazinufaisha jamii.

Kauli hiyo imetolewa Julai 07, 2025 na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Samwel Maneno alipokuwa akizungumza katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere.

oagtanzania



**oagtanzania** NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AHIMIZA UJENZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI UKAMILIKE KWA WAKATI

Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Samwel M. Maneno, amefanya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali linalojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma, leo Julai 10, 2025.

oagtanzania



**oagtanzania** *HABARI PICHA*

Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania (IGP) *Camilius Wambura* tarehe 6 Julai, 2025 ametembelea Banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya 49 ya Biashara ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inashiriki maonesho hayo kwa kutoa huduma ya Elimu ya Sheria, Ushauri wa Kisheria, Kughulikia Malalamiko na Utatuzi wa Migogoro, ambapo Banda la Ofisi liko katika *Mtaa wa Media, Hema la Jakaya Kikwete banda namba 24.*

# MITANDAONI
## 06/07/2025

oagtanzania




View insights

Boost post

29 1

Liked by **leilamuhaji** and others

**oagtanzania** HABARI PICHA

Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bw. Onorius Njole tarehe 6 Julai 2025 ametembelea banda la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Maonesho ya Biashara ya 49 ya Sabasaba yanayoendelea katika Viwanja vya Sabasaba Jijini Dar es Salaam.

Mwandishi Mkuu wa Sheria alipokelewa na Mkurugenzi wa Divisheni ya Uratibu na Ushauri wa Kisheria Bi. Neema Ringo.

# MITANDAONI
## 11/07/2025

**oagtanzania**
Edited · 14h



**oagtanzania** HABARI PICHA

Wakili wa Serikali mkoa wa Arusha , Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bi. Veritas S. Mlay amemwakilisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Hamza S. Johari katika ufunguzi wa Kongamano la Watunga Sera na wadau wa Sekta ya Hifadhi ya Jamiii Barani Afrika (Africa Social Security Association - ASSA)

# MITANDAONI
07/07/2025

oagtanzania



# TUPO KARIBU YAKO!

## Tufuatilie kupitia

oagtanzania

info@oag.go.tz

www.oag.go.tz

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali
Mtaa wa Mtumishi
Mji wa Serikali Mtumba
S. L. P 630
Dodoma - Tanzania

**KWA MSAADA WA HUDUMA ZA KISHERIA PIGA SIMU BURE 0800 11 0188**

Weledi na Ubora